

Kanisa Tukufu

Je! Tufuate Mapokeo au Mafundisho ya Yesu?

Kama tumeona wiki iliyopita mafundisho ya Mungu yalitoka kwa Baba na yalifika hapa ulimwenguni kupitia Yesu. Halafu Yesu aliahidi Msaidizi au Roho Mtakatifu atashuka na kukumbusha maneno ya Yesu. Na ndivyo ilivyotokeo katika Mdo. 2. Halafu wale mitume waliandika maneno au Agano Jipya kupitia Roho Mtakatifu. Kwa hiyo maneno ya Biblia chanzo chake ni Mungu, Baba aliye Mbinguni. Sasa Basi, Tufuate Mapokeo au Maneno ambayo yalishuka kutoka kwa Baba.

- A. Je! Ni nini kuhusu mapokeo na mafundisho ya Kristo?
1. Mapokeo ni nini?
 - a. Mapokeo ni mawazo au mafundisho yalitoka kwa kizazi mpaka kizazi kingine.
 2. Biblia inaongea kuhusu mapokeo sahihi na mapokeo mabaya.
 - a. Mapokeo mabaya-Mt. 15:1-9.
 - b. "Mapokeo mabaya" ni kufundisha mapokeo ya wanadamu kama mafundisho ya _____.
 3. Matokeo ya kufundisha mapokeo mabaya ni nini?
 - a. Mat. 15:1-9 _____.
 - b. Mk. 7:1-13 _____.
 - c. Kol. 2:8 _____.
 - d. Tit. 1:14 _____.
- B. Mapokeo Sahihi.
1. 2 The. 2:15-Tusimame imara na kushika _____.
 2. Kushika mapokeo ya nani?
 - a. 1 Thes. 1:5-9; 2:9-13-Mapokeo sahihi ni maneno ya _____.
- C. Kwa hiyo kama mapokeo yameanzishwa na wanadamu sio yameanzishwa na Mungu. Basi Mungu atayakataa pokeo yo yote yaliyo anzishwa na mwanadamu yo yote.
- D. Kwa hiyo ni muhimu tukumbuke haya kuhusu mapokeo.
1. Uwe mwangalifu kuone mapokeo yametoka kwa Mungu, Mat. 15:1-9.
 2. Uwe mwangalifu kwamba mafundisho yako yametoka kwa Mungu, 1 Tim. 1:3.
 3. Usigeuze injili hata kama malaika anakuambia, Gal. 1:6-9.
 4. Uwe mwangalifu ufikiri zaidi mwanadamu kuhusu Mungu, 1 Kor. 4:3.
 5. Kama mtu anafundisha kinyume na mafundisho ya Yesu, muache, Rum. 16:17-18.
 6. Mifano miwili ya Mapokeo ya wanadamu.
 - a. Kunyunyiza pasipo kuzamisha katika ubatizo-Baraza la Katoliki la Ravenna mwaka wa 1311 bk.
 - b. Vyombo vya Muziki katika ibada-vilianzishwa na Papa Vitilian katika mwaka wa 670 bk.
 - c. Ina maana karibu na miaka 600 na 1300 watu wa Mungu hawakutumia vyombo vya Muziki na kunyunyiza. Lakini sasa je?

Hatimisho:

Tusidanganywe na mwanadamu siku hizi. Mungu alikupa kila kitu ipasacho uzima. Sasa kwa nini tusikilize mtu mwingine. Kufuatana na Ebr. 1:1-2, leo Mungu anaongea nasi kupitia Yesu Kristo TU! Tusifuata akili, hekima au mawazo ya mwanadamu.

Na Robert Stapleton